

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS - TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA**



**MAWASILIANO:**

(i) Mkuu wa shule - 0768-565843  
(ii) Makamu mkuu wa shule - 0764-800 611

**Shule ya Sekondari Usevya**

**S.L.P 528  
Mpanda –**

**Katavi**

**(iii) Mtaaluma Mwandamizi- 0755-714 664 / 0788-268 379**

**22/05/2021**

Mzazi/ Mlezi wa.....

S.L.P .....

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI USEVYA MWAKA 2021/2022.**

1. Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha Tano katika shule hii mwaka wa masomo 2021/2022, tahasusi ya ..... katika Shule ya Sekondari Usevya ambayo ni ya bweni kwa wavulana tu (A'level) inapatikana katika Halmashauri ya (W) Mpimbwe katika, Tarafa ya Mpimbwe, Kata ya Usevya ,Kijiji cha Usevya. Shule ipo umbali wa kilometra 120 Kusini Magharibi mwa mji wa Mpanda. Usafiri wa basi kutoka Mjini Mpanda unapatikana katika kituo cha mabasi Mpanda, nauli ni shilingi elfu Saba (Tsh. 7,000/=). Kama utapitia Sumbawanga, mabasi yanapatikana katika Stendi ya mabasi Sumbawanga. Ukipika Sumbawanga utapanda mabasi ya Majimoto na utashuka kituo cha mabasi Usevya kwa nauli ni shilingi elfu nane (8,000/=) tu. Kwa wanaotokea Dar es Salaam watapanda Magari ya kwenda Mbeya au Sumbawanga moja kwa moja. Ukipika Mbeya utapanda mabasi ya kwenda Sumbawanga na ukifika Sumbawanga utapanda basi linalokwenda Majimoto na kushuka kituo cha mabasi cha USEVYA. Na kwa wanaotokea mikoa ya Kilimanjaro na Arusha watapanda gari linalokwenda Mpanda kupitia Mkoa wa Tabora na kushuka Mpanda mjini. Usafiri wa basi kutoka Mpanda Mjini hadi Majimoto unapatikana katika kituo cha mabasi Mpanda Mjini kwa kupanda mabasi yaendayo Majimoto na utashuka kituo cha mabasi USEVYA, nauli ni shilingi elfu saba (TSh. 7,000/=) tu. panda. Kwa wanaotokea Mwanza watapanda basi linalokwenda Sumbawanga kupitia Tabora na kuendelea na safari hadi Inyonga na Majimoto na kushukia kituo cha mabasi USEVYA kilichopo umbali wa kilometra moja (1) kutoka Shulen. Kutoka hapo unaweza chukua pikipiki (bodaboda) kwa shilingi elfu moja au unaweza kuja kwa miguu hadi shulen.

➤ Muhula wa masomo unaanza tarehe 05/07/2021 Hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shulen kuanzia tarehe 03/07/2021. Mwanafunzi atakae shindwa kufika shule ndani ya muda wa wiki moja tokeea shule kufungua nafasi yake itachukuliwa na mwanafunzi mwingine

## **2. Mambo muhimu ya kuzingatia: -**

### **2.1 Sare ya shule;**

- a) Suruali za bluu nyeusi (dark blue) mbili (2) pamoja na mashati meupe ya mikono mirefu mawili (2). Mshono wa suruali ni wa kawaida usio na malinda na wala isiwe ni nyembamba chini yaani "**modo**" bali iwe na upana wa inchi 18 chini.
- b) Tai za rangi ya bluu nyeusi mbili ambazo ni za kufungwa na sio za kuva, ziwe ndefu.
- c) Viatu vyeusi vya ngozi vya kufungwa na kamba vyenye visigino vifupi.
- d) Soksi za shule jozi mbili (2) ziwe za rangi nyeusi.
- e) Mkanda wa kuvalia suruali uwe wa ngozi wenye rangi nyeusi.
- f) Sweta la rangi ya bluu nyeusi (dark bluu)
- g) Sare ya michezo kwa shule hii ni:-
  - (i) Tahasusi za Sayansi (CBG na PCB) bukta na fulana za rangi nyeusi.
  - (ii) Tahasusi za sanaa (HGK, HGL na HKL) bukta na fulana za rangi nyekundu.
  - (iii) Viatu vya michezo rangi yoyote.
- h) Nguo za kushindia (shamba dress) ni truck suit za rangi ya Bluu na fulana za dark blue (zote zinapatikana shulen) njoo na pesa.

**NB: Mavazi mengine ambayo hayakutajwa hapo juu hayaruhusiwi shulen.**

### **2.2 Ada na michango ya shule.**

(a). Ada ya shule ni shilingi elfu sabini (70,000/=) tu kwa mwaka.unaweza kulipa kiasi cha shilingi 35,000/= kwa muhula au kulipa ada yote kwa mara moja. Fedha hizo zilipwe kwenye akaunti ya shule **Na. 6191200083** katika benki ya NMB, jina la akaunti ni USEVYA SEC. SCHOOL CAPITATION ACCOUNT. |(Tafadhali andika jina la mwanafunzi kwenye Pay in Slip.

- (b) Michango mingine inayotakiwa kulipwa na kila mwanafunzi ni:-
  - i. Shilingi 15,000/= kwa ajili ya ukarabati wa samani za shule.
  - ii. Shilingi 6,000/= kwa ajili ya kitambulisho na picha
  - iii. Shilingi 20,000/= kwa ajili ya taaluma
  - iv. Shilingi 30,000/= kwa ajili ya kuwalipa wapishi, walinzi na vibarua wengine.
  - v. Shilingi 2,000/= kwa ajili ya nembo ya shule.
  - vi. Shilingi 10,000/= kwa ajili ya matibabu (huduma ya kwanza Tsh.5,000/=) na bima ya Afya Tsh. 5,000/=)
  - vii. Shilingi 20,000/= kwa ajili ya mitihani ya kujipima (Mock)
  - viii. Fedha ya tahadhalii shilingi 5,000/= (haitarejeshwa)
  - ix. Shilingi 10,000/= kwa ajili ya maji na umeme
  - x. **Jumla ya ada na michango kwa mwanafunzi ni Shilingi 188,000/=**

(c) Mahitaji mengine ambayo mwanafunzi anapaswa kuleta shulen ni:-

- i. Ream mbili za karatasi A4 kwa mwaka.
- ii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika (orodha imeambatanishwa)
- iii. Madaftari makubwa Counter books Quire 3 yasiyopungua 8
- iv. Wanafunzi wa tahasusi za sayansi PCB na CBG waje na Scientific calculator, Dissecting Kit na koti la maabara (laboratory coat) kwa ajili ya masomo kwa vitendo wawapo maabara.
- v. Godoro moja la futi  $6 \times 2\frac{1}{2}$
- vi. Mashuka mawili (2) rangi ya Bluu bahari (light blue), blanket moja, foronya 1, chandarua 1
- vii. Vyombo vya chakula (sahani 1, bakuli 1, kikombe 1 na kijiko 1)
- viii. Ndoo mbili zenye mifuniko (kubwa 1 na ndogo 1)
- ix. Vifaa vya kufanya usafi.Wanafunzi watatakiwa kuja na vifaa vya usafi kwa mchanganuo ufuatao

(A) Mchepuo wa HKL: jembe 1 na mpini wake na fyekeo 1

(B) Mchepuo wa HGL; Jembe 1, na mpini wake pamoja na ndoo moja (lita 20)

- (C) Mchepuo wa HGK: Mfagio wa ndani (soft broom 1) na mfagio wa nje 1
- (D) Mchepuo wa CBG : Ndoo moja (lita 20) na reki 1
- (E) Mchepuo wa PCB: brashi ngumu 1 na fyekeo 1

**Sisi waalimu tunaamini kwamba mwanafunzi utajitahidi sana kuwa mwanafunzi BORA kwa:-**

- i. Kuwa na nidhamu ya hali ya juu.
- ii. Kuzifahamu na kuzitii sheria za shule na za nchi pia
- iii. Kujiheshimu na kuwaheshimu wanafunzi wenzako,walimu,wananyakazi,viongozi wote wanaozunguka eneo letu
- iv. Kushirikiana na wanafunzi wenzako,Uongozi wa shule ,nchi na wananchi wote wanaozunguka eneo letu
- v. Kujituma (bidii) katika kila jambo unalolifanya
- vi. Kuwa mdadisi/mbunifu katika kujifunza na kuongeza maarifa zaidi pamoja na kuiga mambo mazuri na yenye manufaa katika masomo na maisha yako
- vii. Kuwa nadhifu kimwili,kimavazi na utunzaji wa vifaa vya shule na vifaa vyako vya kujifunzia

Kauli mbiu ya Usevya sekondari ni:- ***USEVYA BILA DIVISION THREE, FOUR NA ZERO INAWEZEKANA. TIMIZA WAJIBU WAKO***

**MATEGEMEO YETU.**

Jumuia ya USEVYA Sekondari inategemea kwamba mwanafunzi:

Utatumia muda wako wa miaka miwili vizuri kwa kujipanga kufaulu kwa; Division I na II, Division III, IV na 0 si mahali pake hapa, hivyo:

- i. Utajiwekea malengo.
- ii. Utahudhuria vipindi vyote vya darasani.
- iii. Utauliza maswali na kushiriki mijadala.
- iv. Hutatoroka vipindi na kwenda kulala bwenini bila sababu maalum au sick room bila kibali cha daktari.
- v. Utajisomea kwa bidii.
- vi. Utaandika nukuu za masomo (notes).
- vii. Utafanya mazoezi (exercises), majoribio (tests) na mitihani yote ya nje (external exams) na ya ndani (internal exams).
- viii. Utatafuta msaada kimasomo kwa wengine kwa mada zitakazokusumbua.
- ix. Utatumia muda wako kwa uangalifu.
- x. Utazingatia kanuni/sheria za shule.
- xi. Utajiheshimu na kuwaheshimu wengine.
- xii. Utaacha anasa zote ikiwemo matumizi ya simu kwa hiari.
- xiii. Usipofanya haya, maana yake unajiandaa kufeli au kufaulu kwa kubahatisha.

**3. MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE.**

- i. Wizi
- ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/ utoro.
- iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo.
- iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake au walimu/ walezi na jamii kwa ujumla.
- v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeoyote yule.
- vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shulenii au kusuka nywele kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule.
- vii. Kufuga ndevu.
- viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevyia.
- ix. Uvutaji wa sigara.
- x. Uasherati, uhusiano wa jinsia moja, kuoau kuolewa.
- xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba.
- xii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja seria za nchi.
- xiii. Kusababisha mimba au kumpa mimba msichana.

- xiv. Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni.
- xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule.
- xvi. Kudharau bendera ya Taifa.
- xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu, n.k.
- xviii. Uharibifu wa mali ya Umma kwa makusudi.

#### **4. Viambatisho na Fomu Muhimu**

- a) Fomu ya uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya serikali. **TAFADHALI NI MUHIMU SANA KUPIMA AFYA YAKO NA KUJA NA VYETI ILI KUONDOA USUMBUFU.**
  - b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi/ mkataba wa kutoshiriki katika mgomo, fujo na makosa ya jinai.
  - c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na kulipa ada, michango na maelekezo mengine yatakayo tolewa na shule.
  - d) Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na namba zao za simu.
5. Tafadhari soma kwa makini maelekezo/ maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.
6. **MWANAFUNZI LAZIMA AJE NA RESULTS SLIP YA MATOKEO YA KIDATO CHA NNE ORGINAL NA SIO KIVULI PAMOJA NA CHETI CHA KUZALIWA.**

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

.....

PATRICK K. NZOWA

MKUU WA SHULE

#### **6. KIAMBATA 'A'**

##### **ORODHA YA VITABU VYA MASOMO WANAVYOTAKIWA KUNUNUA WAZAZI**

Kwa sababu shule hii ina uhaba wa vitabu, ikiwezekana ni vizuri aje na vitabu vitakavyomsaidia kwa masomo husika kati ya vilivyoordheshwa hapa chini: -

##### **a) VITABU VYA HISTORIA: -**

##### **READING LIST FOR HISTORY ONE**

1. Webster J.B. The Growth of African Civilization, the Revolutionary Years of West Africa Since 1800, Longman Press.
2. Walter Rodney, How Europe Underdeveloped Africa.
3. Hallert, R. (1983). Africa Since 1875 Vol.3. East African Educational Publishers. Nairobi, Kenya.
4. July, R.W. (1992). A History of the African People, East African Educational Publishers, Nairobi, Kenya.
5. Illife, J. (1995). Africans, the History of the Continent. Edinburg, Cambridge; University Press, London UK.
6. Manning, P. (1990). Slavery and African Life; Occidental Oriental and African Slave trade, Cambridge University Press.
7. Njiro, E. (1989). A History of Africa in the 19 th century. Literature Bureau Nairobi, Kenya.
8. Rodney, W. (1976). How Europe underdeveloped Africa, Publishing House, Dar es salaam, Tanzania.
9. Shillington, K. (2004). History of Africa. MacMillan Publishers. Hong Kong, Japan.
10. Davidson, E. et al (1997); The growth of the African civilization East and Central Africa to the late 19 th century, Longman Group Limited, Singapore.
11. Freud, B. (1998): The making of contemporary Africa; The Development of African societies since 1800, Colorado, Lynne Rienner Publishers.

12. Kimambo, I and Temu, A (1969); A History of Tanzania, East Africa Publishing House Nairobi, Kenya.
13. Robin, H. (1993); African since 1875 A modern History, East African Publishers Ltd, Nairobi, Kenya.
14. Roland, O. and Anthony, A. (2007). Africa since 1800, Cambridge University Press, New York, USA.
15. History for Secondary Schools Form five (Tanzania Institute of Education)
16. History for Secondary Schools Form Six (Tanzania Institute of Education)
17. History for secondary schools: Form Five (TIE).
18. History for Secondary Schools: Form Six (TIE)

#### **READING LIST FOR HISTORY TWO**

19. Nelson throne Essential modern world history
20. History of 21 st century (World history) (Oxford)
21. H.L. Peacock. A History of Modern Europe 1789-1981 seventh Edition (2010)
22. The History of Modern World (2007) 6 th Edition by Oxford University Press.

**b) VITABU VYA KISWAHILI: -**

1. J.A. MASEBO na M. Nyangwine, Nadharia ya Kiswahili Kidato cha Tano na Sita.
2. H. J.M. Mwasiko, R.D.K. Mekacha, D.L. Masoko, P.C.K. Mtengwa; Kitanglizi cha Tafsiri Nadharia na Mbinu.
3. Tahakiki kidato cha tano na sita.
4. Nadharia ya Fasihi kidato cha tano na sita Kiswahili II.
5. Kiswahili – I: Mwandishi Masuko Christopher Saluhaya.
6. Kitangulizi cha Tafsiri, Nadharia na Mbinu. Wandishi: - H.J.M. Mwansoko, R.D.K. Makacha, S.L.W. Masoko, P.C.K. Mtengwa.
7. Kiswahili Sekondari – Kidato cha Tano (TIE)
8. Kiswahili Sekondari – Kidato cha Sita (TIE)

**9. VITABU VYA UCHAMBUZI**

**USHAIRI**

- Kimbunga - H. Goro
- Fungate ya uhuru - M.S. Khatibu
- Chungu tamu - T.A. Mvungi

**RIWAYA.**

- Vuta n'kuvute - S.A. shafi
- Usiku utakapokwisha - M. Msokile
- Mfadhili - H. Tuwa

**TAMTHILIYA**

- Morani - E. Mbogo
- Nguzo mama - P. Muhando
- Kivuli kinaishi - S. Mohamedi

**c) VITABU VYA JIOGRAFIA:**

1. Pritchard J.M. (1979), Africa a study Geography for Advanced students London Longman.
2. Msabila D. T (2003) Success in Geography climatology and Soil Science Dar es salaam – Afroplus Industries L.T.D.
3. Prichard J.M. (1990) Practical Geography for Africa, Longman.
4. Kamili, A Comprehensive Approach Practical Geography For Advanced Level, Dar es salaam, Afroplus Industries.
5. Kamili, Physical Geography for Africa, Dar es salaam Afroplus Industries.
6. Msabila D.T. Physical Geography, Dar es salaam Nyambari Nyangwine Publishers.
7. Msabila D.T. (2006) Human and economic Geography (Advanced level paper 2) Nyambai Nyangwine publishers.

**d) VITABU VYA LANGUAGE (1) ONE: -**

1. Nichlolus arshery, Comprehensive English Grammar New edition.

2. Michael Kadeghe, Semantics phonology and styhstics. (blue).
3. Ashel, N. (2009) Advanced Level English A Practical Approach. DSM.
4. Kadeghe, Michael (2011) The real English Textbook for Advanced Level (form Six) – DSM
5. Kadeghe, Michael (2011) The real English Textbook for Advanced Level (form five) – DSM.
6. English Language for Secondary Schools, Language & Usage – Form Five & /six (TIE) papers.
7. Advanced English Language: Form Five & Six by Oxford.

**e) LANGUAGE (II)**

1. Ashel, N. (2011), Advanced Level Literature. The Essential Guide; Good Book Publishers, DSM.
2. Advanced Level Literature, (2008), Nyambui Nyangwine Publishers, DSM.
3. Achebe, A. (1966) A man of the People.
4. Ayi Kwei Armah (1968), The Beautiful Ones Are Not Yet Born.
5. Ibsen, H. (1882), An Enemy of the People, EA-DSM
6. Imbuga, FC (1976) Betrayal in the City.
7. Mirii Ngugi & Thing'ol (1982), I Will Marry When I Want, EAEP, DSM.
8. Institute of Education, Selected Poems.
9. Mloka, C. (2007) The Wonderful Surgeon.
10. English Language for Secondary Schools, Literature & Stylistics – Form Five & Six (TIE). Paper 2.

**f) GENERAL STUDIES: -**

1. General studies Approach.
2. Richard, R.F. Mbalase. General Studies for Advanced Level Certificate;
3. Mgaywa, B.M. General Studies for Advanced level 3 rd Ed.
4. Joannes Bigirwa Mungu & Sospeter. M. Deogratias. Understanding Advanced Level general Studies; Advance Secondary SchoolEducation;

**g) VITABU VYA FIZIKIA**

1. S.CHAND–Conceptual physics XI na XI
2. NELKON AND PARKER PHYSICS
3. RANSDEN PHYSICS

**h) VITABU VYA KEMIA**

1. By S.chand,Conceptual Chemistry for class X land XII
2. By Tanzania Institute of Education, ADVANCED LEVEL INORGANIC CHEMISTRY part I and II.
3. Advanced chemistry review (2000-2012) 4.Ramsden, E.M (2000) A- level Chemistry, 4<sup>th</sup> Edition II.

**i) VITABU VYA BIOLOJIA**

1. By Tayloratel (1999) Biological Science, third edition.Tong printing press Hongkong.
2. By Glenn and Tod,s (1999) Understanding Biology 4th Ed.Stanlye Thomes Ltd UK

**h) Fedha ya matumizi binafsi na nauli ya kurudia nyumbani wakati wa likizo**

Niwayibu wa kila mzazi/mlezi kuhakikisha kwamba anampatia mtoto wake fedha za kutosha kwa ajili ya matumizi binafsi pamoja na nauli ya kurudi nyumbani wakati wa likizo.

**KIAMBATA 'B'**

FOMU YA TAARIFA BINAFSI YA MWANAFUNZI, KUKUBALI SHERIA ZA SHULE NA NAFASI YA SHULE ALIYOPEWA

A. TAARIFA BINAFSI YA MWANAFUNZI (liazwe na mwanafunzi):

1. Jina kamili la mwanafunzi \_\_\_\_\_
2. Tahasusi \_\_\_\_\_ Jinsia (Me/ Ke) \_\_\_\_\_ Uraia \_\_\_\_\_
3. Kabilia \_\_\_\_\_ Dini \_\_\_\_\_ Kanisa / msikiti anakosali ni \_\_\_\_\_
  
4. Tarehe ya kuzaliwa \_\_\_\_\_
5. Mahali alipozaliwa: Kitongoji/ mtaa \_\_\_\_\_ Kijiji \_\_\_\_\_  
Kata \_\_\_\_\_ Tarafa \_\_\_\_\_ Wilaya/Mji \_\_\_\_\_

*Picha ya  
Mwanafunzi*

Mkoa \_\_\_\_\_

6. Yatima / Sio yatima \_\_\_\_\_ Amempoteza \_\_\_\_\_

7. Historia ya Shule alizosoma kabla ya kuja Sekondari ya Usevya

(a) S/M MSINGI:

JINA LILIOANDIKISHWA SHULENI SHULE YA MSINGI.....

ALIKOTOKA.....

TAREHE NA MWAKA ALIOANZA.....

TAREHE NA MWAKA ALIOTOKA/ MALIZA.....

1. (B) SEKONDARI:

JINA LILIOANDIKISHWA SHULENI SHULE YA SEKONDARI.....

TAREHE NA MWAKA ALIOANZIA.....

TAREHE NA MWAKA ALIOTOKA/ MALIZA.....

8. Namba ya Mtihani (CSE); \_\_\_\_\_ Shule niliyofanya kidato cha nne; \_\_\_\_\_

Wilaya ya \_\_\_\_\_ Mkoa wa \_\_\_\_\_

### B. KUKUBALI NAFASI NA MAELEKEZO ULIYOPEWA.

MIMI ..... KIDATO CHA ..... MWAKA ..... MCHEPUO

WA..... Nimesoma na kuyaelewa maelekezo yote. Hivyo nakubali kuipokea/ sikubali kuipokea nafasi niliyopewa. Nathibitisha kwamba nimekubali kuijunga na shule hii kwa hiari na nimepokea maagizo na maelekezo bila kulazimishwa na naahidi kuyazingatia na kutimiza yale ninayopaswa kutimiza bila kulazimishwa. Nitasoma kwa bidii ili nifaulu mitihani yote ya ndani na ya nje.

TAREHE:..... SAINI: .....

### C. KUKUBALI SHERIA ZA SHULE:

#### MWANAFUNZI:

Mimi: ..... wa Tahasusi ya ..... nimezisoma na kuzielewa sheria, taratibu, kanuni na miongozo ya shule iliyomo kwenye fomu hii na nitakayosomewa wakati wa **Orientation course**. Ninaahidi kwamba nitazingatia na kutii masharti, sheria, kanuni, taratibu, miongozo ya shule na maelekezo mengine nitakayopewa na walimu, watumishi wasio walimu na viongozi wote wa shule. Sitashiriki katika mgomo, fujo, wala makosa ya jinai yaliyoorodheshwa hapo juu. Nikivunja au kukiuka maelekezo na sheria yoyote niko tayari kuwajibishwa kulingana na adhabu zilizoorodheshwa kwa kila kosa.

### D. TAARIFA YA MZAZI/MLEZI ;( ANDIKA MAJINA MATATU)

1. JINA LA BABA: .....

JE, BABA YUKO HAI/AMEFARIKI: .....

MAHALI ANAPOISHI: KITONGOJI:..... KIJIJI:..... KATA:.....

TARAFA ..... WILAYA ..... : KAZI YA BABA:.....

SIMU YA BABA ..... S.L.P ..... MJI.....

Picha ya Baba

2. JINA LA MAMA.....

YUKO HAI/AMEFARIKI .....

MAHALI ANAPOISHI: KITONGOJI..... KIJIJI..... KATA.....

TARAFA..... WILAYA..... KAZI YA MAMA: ..... SIMU YA

MAMA..... S.L.P..... MJI.....

Picha ya  
Mama

### ENDAPO MWANAFUNZI ANALELEWA NA MLEZI (Ajaze sehemu)

3. JINA LA MLEZI WA KIUME.....

MAHALI ANAPOISHI..... UHUSIANO.....

SIMU:..... S.L. P ..... MJI .....

KAZI ANAYOFANYA ..... MWAJIRI .....

Picha ya  
Mlezi  
wa Kiume

4. JINA LA MLEZI WA KIKE.....  
MAHALI ANAPOISHI .....UHUSIANO.....  
SIMU.....S.L.P.....MJI.....  
KAZI ANAYOFANYA .....MWAJIRI .....

*Picha ya Mlezi  
wa Kike*

**E. MZAZI/MLEZI (Azaje Sehemu Hii):**

Mimi..... nikiwa Mzazi/Mlezi nimezisoma sheria na maagizo mengine ya shule yanayomhusu mwanafunzi.....na ninaahidi kutimiza wajibu wangu kama Mzazi/Mlezi wa mtoto huyu kwa: kumshauri ipasavyo ili awe mwanafunzi mwenye nidhamu na ufaulu mzuri. Pia naahidi kulipa ada ya shule na michango itakayokubaliwa na kumtimizia mahitaji yake ya shule. Nitahudhuria vikao vya shule kwa kadri vitakavyokuwa vinaitishwa na endapo sitahudhuria nitakubaliana na maamuzi yatakayokuwa yametolewa na nitawajibika kulingana na maamuzi hayo.

TAREHE:..... SAINI: .....

**F: SEHEMU YA NDUGU WA KARIBU:**

Ndugu wa karibu wanne (4) wanaoruhusiwa kumtembelea mwanafunzi anapokuwa shulenii.

Majina matatu mfano: ROSE ZABRON MUSSA.

JINA	UHUSIANO	NAMBA ZA SIMU:
1. ....	.....	.....
2. ....	.....	.....
3. ....	.....	.....
4. ....	.....	.....

**12. KIAMBATA 'C'**

**THE REPUBLIC OF TANZANIA  
PRESIDENT'S OFFICE  
REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT  
MPIMBWE DISTRICT COUNCIL**

**PART A:****REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**

TO: Medical Officer FROM: THE HEADMASTER  
USEVYA SECONDARY SCHOOL.  
P O BOX 528  
MPANDA-KATAVI

Please examine the above named as to his/her physical and mental fitness for a full time academic studies.

- A: 1. (a) Eye -sight (b) Hearing (c) Speech (d) Veneral Disease (e) Leprosy (f) Limbs (g) Epilepsy  
2. Neuroses  
3. Other serious diseases

B: BLOOD GROUP \_\_\_\_\_

**PART: B FOR MEDICAL EXAMINATION**

(To be completed by Government Medical Officer)

I have examined the above named student that he/she is physically fit/unfit and mentally \*fit/unfit for a full time academic studies at your school.

- (a) Eye-sight.....  
(b) Hearing .....,  
(c) Speech.....  
(d) Veneral disease.....  
(e) Leprosy .....  
(f) Limbs .....,  
(g) Epilepsy.....  
(h) Neurosis.....  
(i) Pregnancy .....,  
(j) Other serious diseases.....  
(k) BLOOD GROUP .....

DATE ..... SIGNATURE ..... OFFICIAL STAMP.....

**13 . SHERIA ZA SHULE: -****A). MIPAKA YA SHULE.**

a) Mwanafunzi haruhusiwi kutembelea vijiji jirani wala kwenda mjini bila kupata kibali cha Mkuu wa Shule/makamu mkuu wa shule au Mwalimu yeyote.

b) Mwanafunzi haruhusiwi kwenda kwenye nyumba za wafanyakazi wa shule bila idhini ya Mkuu wa Shule.

**B). MAVAZI RASMI YA SHULE****1. DARASANI:**

- a) Suruali ya bluu nyeusi na shati jeupe la mikono mirefu kwa kidato cha tano na sita.  
b) Viatu vyeusi vyakama visivyo na visigino virefu na visiwe vyakama kugonga.  
c) Soksi bluu nyeusi

**2. KAZINI: -** Mwanafunzi anatakiwa kuvali suruali ya track na T-shirt ya Tanzania awapo kazini.

**3. MICHEZONI: -** Mwanafunzi awapo michezoni avae nguo za michezo kama zilivyo ainishwa hapo juu.

**4. NJE YA SHULE: -** Mwanafunzi akiwa nje ya Shule avae suruali ya shule pamoja na Tshirt ya shule yenye nembo.

**5. SAFARINI:** - Mwanafunzi anapokuwa safarini avae suruali ya shule pamoja na T-shirt ya shule yenye nembo.

## **6. UTARATIBU KATIKA BWALO LA CHAKULA**

- (a) Ni muhimu kufuata utaratibu na saa zilizopangwa za kula kufuatana na ratiba ya shule.
- (b) Kila mwanafunzi awe na sahani, bakuli, kijiko na kikombe. Vyombo hivi vitunzwe bwenini.
- (c) Wanafunzi wakae mezani wakati wa chakula.
- (d) Wanafunzi hawaruhusiwi kupiga kelele wakati wa chakula.
- (e) Mwanafunzi haruhusiwi kuingia na ndala au kiatu cha wazi (sandals) AU kandambili ndani ya bwalo la chakula.

## **7. JIKONI**

- (a) Wanafunzi hawaruhusiwi kuingia jikoni wala kujipikia vyakula kama wanavyotaka.
- (b) Viranja wa zamu na viongozi wa meza ndio wanaoruhusiwa kuingia jikoni wakati wa kupakua chakula.

## **8. MABWENINI**

- (a) Wanafunzi hawaruhusiwi kulala wawili kitanda kimoja.
- (b) Kila mwanafunzi ni lazima alale katika bweni na chumba alichopangiwa.
- (c) Wanafunzi hawaruhusiwi kuongea, kutembea mabwenini au nje ya bweni baada ya saa 5:00usiku.
- (d) Ni marufuku kupiga na kusikiliza muziki bwenini.
- (e) Upotevu/uharibifu wowote wa mali ya umma bwenini utoalipwa na wakazi husika wa bweni.
- (f) Mwanafunzi haruhusiwi kuwepo bwenini wakati wa masomo au wakati ratiba ya shule ikiendelea.
- (g) Mwanafunzi haruhusiwi kuingia na chakula au kula chakula bwenini.
- (h) Kila mwanafunzi azingatie usafi wa bweni siku zote na siku maalumu za usafi.

## **9. DARASANI**

- (a) Wanafunzi wawe madarasani mnamo saa mbili asubuhi.
- (b) Mwalimu anapoingia darasani wanafunzi wasimame na kuamkiana na mwalimu.
- (c) Wanafunzi wasipige kelele wawapo darasani.
- (d) Wanafunzi wasitoke nje ya darasa wakati wa masomo bila ruhusa maalumu.
- (e) Ni wajibu wa kila mwanafunzi kujibu na kuuliza maswali na kukamilisha kazi alizoachiwa na mwalimu wa somo.
- (f) Usafi wa darasani ni wajibu wa kila mwanafunzi.

## **10. NJE YA DARASA**

- (a) Wanafunzi wasimamae na kumsalimu mwalimu au mtu aliywazidi umri kila anapopita.
- (b) Wanafunzi wawaheshimu wafanyakazi wengine waliopo shulen kama inavyostahili.
- (c) Wanafunzi watumie lugha ya heshima kwa walimu, watu wengine na hata wao kwa wao.
- (d) Wanafunzi wawe watii, wasiwe wagomvi, wasengenyaji, wavivu, walevi na wazururaji.
- (e) Wanafunzi wawe na moyo wa kushirikiana na kusaidiana wakati wa shida na raha.
- (f) Wanafunzi waheshimu bendera ya taifa na ukumbi wa mikutano.
- (g) Wanafunzi hawaruhusiwi kusomea nje ya madarasa, mabwenini au bwaloni.
- (h) Mwanafunzi ataongea kiingereza wakati wote awapo shulen.

## **11. MATIBABU**

- (a) Wagonjwa wote watatibiwa katika hospitali ya serikali ya wilaya pamoja na kituo cha afya Usevya tu.
- (b) Shule itagharamia matibabu kwa gharama ya hadi elfu 10,000/= tu na zaidi ya hapo mzazi au mlezi atalazimika kufidia gharama zinazooen gezeka.

## **12. MAK TABA YA SHULE**

- (a) Wanafunzi hawaruhusiwi kuingia maktaba wakiwa wamebeba mikoba ya vitabu/ madaftari.
- (b) Wanafunzi waingie maktaba wakiwa wamevaa vazi rasmi la shule.
- (c) Mwanafunzi haruhusiwi kutoka nje ya maktaba na kitabu au gazeti bila ruksa ya mkutubi au mwalimu mhusika na maktaba.

(d) Mwanafunzi ataingia maktaba katika muda maalumu uliopangwa tu.

### **13. WAGENI**

- (a) Wageni wa aina yoyote ile hawaruhiwi kuingia au kupita shulenii bila shida maalumu na idhini ya mlinzi au mwalimu wa zamu.
- (b) Wageni wa aina yoyote ile hawaruhusiwi kuonana na wanafunzi isipokuwa kwa wale wenye shida za kiofisi tu kupitia kwa mwalimu wa zamu
- (c) Maagizo yote ya wageni kwa mwanafunzi au wanafunzi yatapokelewa na mwalimu wa zamu (vyakula na vinywaji kama pombe na dawa za kienyeji havitapokelwa).

### **14. HUDUMA ZA OFISI**

- (a) Ofisi ya shule ndiyo itapokea taarifa za dharura za wanafunzi kama vile msiba au tatizo kubwa la kifamilia pamoja na maagizo yote ya wazazi/walezi kwa mwanafunzi.
- (b) Mwanafunzi haruhusiwi kupiga au kupokea simu bila idhini ya Mkuu wa shule.
- (c) Wanafunzi wanaruhusiwa kuingia ofisi yoyote shulenii isipokuwa ni lazima wagonge/ wapige hodi kabla ya kuingia.
- (d) Barua za wanafunzi zitapokelewa na mwalimu wa zamu ambaye atazikabidhi kwa kiranja wa zamu ili azigawe kwa wahusika.

### **15. MAMBO YASIORUHUSIWA KUFANYA**

- (a) Uasherati
- (b) Wizi
- (c) Kuchezea au kuharibu bendera ya taifa.
- (d) Kugoma adhabu
- (e) Kumpiga au kumtukana mwalimu/mfanyakazi
- (f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
- (g) Kutoroka shule au kuachana na wenzako wakati unapotoka nje ya shule kwa shughuli za kishule.
- (h) Kunywa au kulewa pombe/kuvuta sigara au bangi
- (i) Kupiga/ Kupigana
- (j) uzururaji
- (k) Kupiga kelele ovyo au kuita kwa sauti kubwa.
- (l) Ubaguzi wa aina yeoyote
- (m) Kuzungumza lugha nyininge yoyote isipokuwa kiingereza (Kiswahili kinaruhusiwa katika mazingira maalumu tu)
- (n) Kuвая mavazi yasiyo sare ya shule
- (o) Kutofika au kuchelewa sehemu ya parade
- (p) Ni marufuku kwa mwanafunzi kuja na simu, kamera pamoja na radio shulenii.
- (q) Mwanafunzi anatakiwa kuja na namba mbili za simu ambazo zitasaidia kupata mawasiliano ya wazazi/mlezi.

**16. Elewa kuwa si rahisi kutunga sheria za kila kosa linaloweza kufanywa na mwanafunzi. Sheria ni mwongozo wa kumwelewesha mwanafunzi mambo ambayo haruhusiwi kuyafanya. Kitu muhimu ni kwamba kila mwanafunzi atumie akili yake na busara kuweza kujua namna gani ya kuishi na walimu pamoja na wanafunzi wenzake ili kutumia nafasi yake kujipatia elimu na kuishi kwa raha na amani katika jitihada za kuijendeleza mwenyewe, shule pamoja na taifa zima.**

Kumbuka kuwa umepata bahati kubwa kuwa kati ya wanafunzi waliochaguliwa kuijunga na shule hii kwa hali hiyo toa mchango wako katika kujenga msingi imara, sifa na mwenendo mzuri na maendeleo safi kwashule yako ya Usevya.

**KARIBU SANA**